


JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



MWELEKEO WA HALI YA HEWA KWA TANZANIA
KIPINDI CHA JUNI - AGOSTI (JJA), 2018



Dondoo muhimu za hali ya hewa kipindi cha Juni-Agosti (JJA), 2018

Taarifa hii inatoa uchambuzi wa mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa, joto, upepo na mvua katika kipindi cha miezi ya Juni hadi Agosti (JJA), 2018: ushauri na tahadhari kwa wadau wa sekta mbalimbali wanaotumia taarifa za hali ya hewa katika utekelezaji wa majukumu yao. Kwa muhtasari, mwelekeo huo na athari zake unaonesha kuwa:

a) Viwango vya chini vya joto

- Katika kipindi cha JJA, 2018 hali ya joto la wastani hadi chini ya wastani inatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi. Hata hivyo, hali ya baridi inatarajiwa katika maeneo ya miinuko ya nyanda za juu Kaskazini mashariki (Arusha, Kilimanjaro na Manyara), Nyanda za juu kusini Magharibi (hususani mkoa wa Njombe) pamoja na maeneo ya miinuko ya mkoa wa Tanga (hususani wilaya za Lushoto na Bumbuli).

b) Mvua na Upepo

- Maeneo mengi yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla, vipindi vifupi vya upepo mkali vinatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo. Hata hivyo, vipindi vya mvua za nje ya msimu vinatarajiwa katika maeneo ya pwani hususan katika wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Juni, 2018 na vipindi kadhaa kwa mwezi Julai, 2018.

c) Athari

- Hali ya baridi inayotarajiwa katika maeneo mengi ya nchi hususan maeneo ya miinuko inaweza kusababisha kudumaa kwa mazao kama vile ndizi pamoja na mazao ya nje ya msimu, na kuathiri mifugo.
- Kutokana na hali ya joto katika bahari ya Hindi kuwa juu ya wastani kiasi, ongezeko la siku zenye tija katika shughuli za uvuvi katika kipindi cha msimu wa JJA linatarajiwa.

1.0 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Hali ya joto la bahari la wastani inatarajiwa katika eneo la ukanda wa kati wa kitropikali wa bahari ya Pasifiki katika kipindi cha msimu wa JJA, 2018. Aidha, kusini magharibi mwa bahari ya Hindi joto la bahari linatarajiwa kuwa la juu ya wastani, wakati joto la bahari la juu ya wastani hadi wastani linatarajiwa mashariki mwa bahari ya Hindi. Joto la bahari katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki linatarajiwa kuwa chini ya wastani hadi wastani. Hali hii inatarajiwa kusababisha upepo kuvuma kutoka magharibi. Joto la bahari la wastani hadi chini ya wastani linatarajiwa katika eneo la ncha ya kusini ya bara la Afrika hivyo kusababisha msukumo wa wastani wa upepo wa kusi katika kipindi cha msimu wa JJA, 2018.

2.0 MATARAJIO YA VIWANGO VYA CHINI VYA JOTO KWA MIEZI YA JUNI HADI AGOSTI, 2018

Kwa kawaida msimu wa JJA, ni msimu wenye hali ya vipindi vya baridi na ukavu. Katika msimu huu joto linatarajiwa kuwa la wastani katika maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki, Ziwa Victoria, magharibi, mikoa ya kati na maeneo ya mashariki mwa mikoa ya kusini. Hata hivyo, joto linatarajiwa kuwa la wastani hadi chini ya wastani katika maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi na magharibi mwa mikoa iliyopo kusini. Aidha, joto linatarajiwa kuwa la wastani hadi juu ya wastani katika maeneo ya ukanda wa pwani. Viwango vya joto vinavyotarajiwa hususan nyakati za usiku hadi alfajiri katika maeneo mbalimbali ya nchi ni kama ifuatavyo:

2.1 Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Mwanza, Mara, Geita, Kagera, Shinyanga na Simiyu):

Kiwango cha chini cha joto kinatarajiwa kuwa *kati ya nyuzi joto 14 na 18* katika maeneo mengi. Hata hivyo, kiwango cha joto cha chini ya nyuzi joto 14 kinatarajiwa katika maeneo ya miinuko hususan katika mikoa ya Kagera na Geita.

2.2 Ukanda wa pwani ya kaskazini (Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Tanga, maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):

Kiwango cha joto kinatarajiwa kuwa *kati ya nyuzi joto 18 na 24* katika maeneo mengi. Hata hivyo, vipindi vya baridi vinatarajiwa katika maeneo ya miinuko ya mkoa wa Tanga hususan wilaya za Lushoto na Bumbuli ambapo kiwango cha chini ya nyuzi joto 18 kinatarajiwa.

2.3 Kanda ya nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):

Katika msimu huu kwa ujumla kiwango cha joto kinatarajiwa kuwa *kati ya nyuzi joto 12 na 17* katika maeneo mengi. Hata hivyo, katika maeneo ya miinuko kiwango cha cha joto kinatarajiwa kuwa *chini ya nyuzi joto 12*.

2.4 Kanda ya magharibi (Mikoa ya Kigoma, Tabora na Katavi):

Kiwango cha joto kinatarajiwa kuwa *kati ya nyuzi joto 14 na 16* katika maeneo mengi.

2.5 Kanda ya kati (Mikoa ya Singida na Dodoma):

Kiwango cha joto kinatarajiwa kuwa *kati ya nyuzi joto 12 na 15* katika maeneo mengi, vipindi vichache vya baridi chini ya nyuzi joto 12 vinatarajiwa.

2.6 Ukanda wa pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):


Kiwango cha joto kinatarajiwa kuwa *kati ya nyuzi joto 19 na 24* katika maeneo mengi.

2.7 Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):

Kiwango cha joto kinatarajiwa kuwa *kati ya nyuzi joto 12 na 16* katika maeneo mengi. Aidha, kiwango cha joto katika maeneo ya miinuko kinatarajiwa kuwa chini ya nyuzi joto 12.

2.8 Kanda ya nyanda za juu kusini-magharibi (Mikoa ya Mbeya, Songwe, Iringa, Njombe pamoja na maeneo ya kusini ya mkoa wa Morogoro):

Katika msimu huu, kiwango cha joto kinatarajiwa kuwa *kati ya nyuzi joto 5 na 12* katika maeneo mengi. Aidha, kiwango cha joto katika maeneo ya miinuko kinatarajiwa kuwa chini ya nyuzi joto 5.



Picha 1: Mwelekeo wa viwango vya joto katika msimu wa JJA, 2018.

3.0 MWENENDO WA UPEPO NA MWELEKEO WA MVUA KWA KIPINDI CHA JUNI HADI AGOSTI (JJA), 2018

Kwa kawaida huu ni msimu wa upepo wa *kusi* katika ukanda wa pwani ya bahari ya Hindi. Katika msimu wa mwaka huu, hali hiyo inatarajiwa kuwepo ikiambatana na vipindi kadhaa vya upepo kutoka kusini mashariki katika mwambao wa pwani ya Tanzania.

Pamoja na kwamba kipindi cha msimu wa JJA kwa kawaida huwa ni kikavu, katika Msimu wa mwaka huu, vipindi vya mvua za nje ya msimu vinatarajiwa kujitokeza katika maeneo machache ya visiwa vya Unguja na Pemba, pamoja na ukanda wa Pwani (Mikoa ya Tanga, Dar es Salaam, Pwani na Lindi).

Vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika mikoa ya Kagera, Geita na Mara hususan kwa mwezi Agosti, 2018. Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo ya miinuko hususan (Rungwe (Tukuyu) na Njombe).

4.0 ATHARI NA USHAURI

Hali ya baridi inayotarajiwa katika maeneo mengi ya nchi hususan maeneo ya miinuko inaweza kusababisha kudumaa kwa mazao kama vile ndizi na mazao mengine ya nje ya msimu na kuathiri mifugo. Kutokana na hali ya joto katika bahari ya Hindi kuwa juu ya wastani kiasi, ongezeko la siku zenye tija katika shughuli za uvuvi katika kipindi cha msimu huu linatarajiwa.

Hata hivyo, wananchi na sekta husika wanashauriwa kuchukua hatua stahiki kutokana na athari hasi zinazoweza kuambatana na matarajio ya utabiri huu.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania itaendelea kufuatilia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na kutoa taarifa za hali ya joto na upepo.

Imetolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania: